

EE BWANA MUNGU WANGU

Zab. 30: 1, 3, 5, 10-12

Anga Anselim

Tar. 25, April, 2022

Kibosho Senior Seminary

Con passione

$\text{♩} = 68$

Soprano
Alto

Ee Bwa na Mu ngu wa na ngu

Tenor
Bass

(Bwa na)

1. 2.

Na li ku li li a, (Bwa na) u ni po nye (Bwa na) nye.

1. Ee Bwana, nitakutukuza kwa maana umeniinua,
Wala hukuwafurahisha adui zangu juu yangu./
Umeniinua nafsi ayngu, Ee Bwana kutoka kuzimuni,
Umenihuisha na kunitoa miongoni mwao washukao shimoni.
2. Mwombieni Bwana zaburi, Enyi watauwa wake,
Na kufanya shukrani, kwa kumbukumbu la utakatifu wake./
Maana ghadhabu zake ni za kitambo kidogo,
Katika radhi yake mna uhai,
Huenda kilio huja kukaa usiku, lakini asubuhi huwa furaha.
3. Ee Bwana, usikie, unirehemu, Bwana uwe msaidizi wangu.
Uligeuza matanga yangu kuwa machezo/
Ulinivua gunia, ukanivika furaha.
Ee Bwana, Mungu wangu, nitakushukuru milele.